

# UBAGUZI HAUKUBALIWI KWENYE .....

Watu wote wamezaliwa huru na sawa na wanapaswa kutendewa sawa. Ubaguzi **KAMWE** haukubaliwi.



## UBAGUZI NI NINI?

Tabia yoyote inayotendwa kazini isiyo sawa na inayomtofautisha mtu mmoja na wengine kwa sababu ya sifa za kibinafsi. Mtu yeyote – wanawake na wanaume, wafanyakazi wenza, wasaidizi – wanaweza kumbagua mtu mwingine kazini. Mifano ya kawaida:



*Kuwaachisha kazi wanawake wajawazito au kuwapa majukumu ya malipo ya chini.*

*Mshahara usio sawa kwa wanawake na wanaume katika kazi sawa.*

*Kipimo cha ujauzito kabla ya kuajiriwa au kazini.*

*Kupendelea vikundi fulani kwa uongozi*

## JE, SIFA ZA KIBINAFSI NI ZIPI?

Sifa za kibinafsi ni binafsi. Hazipaswi kutumiwa kuwatendea baadhi ya watu utofauti wakati wa kuomba kazi, au wakiwa kazini, vinginevyo hawatakuwa na fursa sawa. Mifano ya kawaida :



*Umri*

*Jinsia*

*Ulemavu / Ujauzito*

*Kabila / Rangji*

## JE, VITENDO VISIVYOONYESHA UBAGUZI KAZINI NI VIPI?

Vitendo vya KUTOWAPENDELEA watu fulani kwa sababu ya sifa zao za kibinafsi. Vitendo VISIVYOSABABISHA matokeo yasiyofaa au yasiyo ya haki kwa watu kwa sababu ya sifa zao za kibinafsi. Mifano ya kawaida:



*Kuwezesha kazi au huduma kwa makundi ya watu wasiojiweza.*

*Kuwapa wanawake wajawazito kazi nyepesi na malipo sawa.*

*Kumlipa zaidi mtu ambaye kazi zake zina majukumu au wajibu zaidi.*

**JINSI YA KURIPOTI UBAGUZI**  
Ubaguzi unadhuru watu na unadhuru biashara.  
**Ifichue, isuluhishe, ikomeshe!**



Wasiliana na Kamati ya Malalamiko au Kamati ya Kutathmini-na-Kushughulikia au Kamati ya Jinsia au (weka hapa): .....

Wajumbe wa kamati yako ni: .....

Wasiliana na (piga simu/SMS): .....

Visa vya ubaguzi hushughulikiwa na Kamati yako ya Kuathmini-na-Kushughulikia na Kamati ya Jinsia.